**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARIMYA WASICHANA GEITAKATIKA HALMASHAURI YA MJI GEITA MKOA WA GEITA 2024/2025.

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI** .............................................................................................

YAH**:- MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA GEITA**

**HALMASHAURI YA MJI GEITA, MKOA WA GEITA – 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari ya wasichana Geita mwaka **2024/2025**, tahasusi ya **…,** shule ya sekondari ya wasichana Geita ipo mtaa wa Magogo umbali wa kilometa mbili (**2**) kutoka Geita mjini. Ukitokea Mwanza shule ipo mkono wa kulia na ukitokea Geita shule ipo mkono wa kushoto. Nauli ni shilingi **500/=** kwa haice na shilingi **2,000/=** kwa pikipiki kutoka Geita mjini. Muhula wa masomo unaanza tarehe **01.07.2024**. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01.07.2024** au kama ilivyoelekezwa na **OR – TAMISEMI**, mwisho wa kuripoti ni ndani ya wiki mbili toka kuanza kwa mhula yaani **01.07.2024**.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### A. SARE YA SHULE.

**a)** Mashati mawili (02) blue bahari (light blue) yenye mikono mirefu.
**b)** Sketi mbili (02) rangi ya grey, dark blue, maluni na nyeupe kitambaa cha suti Grade one zenye rinda box mbele na nyuma na marinda 2 upande wa kulia na kushoto, mkanda inch 2 na inch 8 kutoka kwenye magoti yaani sketi iwe ndefu. Angalia mfano wa sketi mchoro hapo chini na rangi ya kitambaa.




**Mchoro wa sketi namna ya kushona.**



**Kitambaa cha sketi**

- **c)** Rangi ya tai ifanane na rangi ya sketi
- **d)** Sweta moja ya rangi ya dark bluu yenye mstari mweupe mikononi, shingoni na kiunoni na yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni).
- **e)** Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba kuanzia matundu manne vyenye visigino **BUTU**, (visiwe aina ya facebook)
- **f)** Soksi nyeupe ndefu jozi 02 au zaidi.
- **g)** T-shirt 01 yenye nembo ya shule ya rangi ya bluu yenye kola nyeupe. (Inapatikana shuleni.)
- **h)** Tracksut ya rangi ya kijivu kwa ajili ya night preparation (kujisomea usiku).
- **i)** Tracksut ya rangi ya dark bluu kwa ajili ya michezo.
- **j)** Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo na T-shirt ya bluu (rangi ya Chealsea)
- **k)** Shamba dress 02 (gauni za kushindia) za heshima ndefu mtindo wa solo kitambaa cha rangi ya dark bluu mikono mifupi shingo iwe duara kizito cha suti grade one, sio sukari. Nguo zingine haziruhusiwi.
- **l)** Kizibao cha rangi ya dark bluu.

## B. MICHANGO YA UENDESHAJI WA SHULE.

| S/N. | AINA YA MICHANGO. | KIASI | BENK |
|---|---|---|---|
| 01. | Michango ya uendeshaji wa shule | **65,000/=** | **CRDB** Geita girls' Secondary School. **0150859672600.** **Andika jina la mwanafunzi kwenye BANK PAY SLIP.** |
| 02. | Nembo ya shule | **5,000/=** | |
| 03. | Tahadhali | **5,000/=** | |
| 04. | Kitambulisho | **5,000/=** | |
| **JUMLA ITAKUWA** | | **80,000/=** | |

## C: MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.

- **i.** **R**eam 02 ya karatasi A4 **DOUBLE A** (KWA MWAKA).
- **ii.** Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vya TIE (TAASISI YA ELIMU TANZANIA)
- **iii.** Godoro ft 2½, waweza kuja nalo au ukanunua Kasamwa.
- **iv.** Shuka pair 02 rangi ya pinki, blanketi 01 jepesi, taulo 01.
- v. Mto na foronya yake ya pinki, chandarua 01 nyeupe ya pembe nne.
- vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
- vii. Ndoo 01 kubwa ya lita 20, soft broom 01, hard broom 01,mfagio wa nje wa chelewa 01 **na DAWA YA ARO** chupa 01 kwa ajili ya usafi wa bweni na vyoo kwa wanafunzi wa **PCB.**
- viii. Ndoo 01 ndogo lita 10 rangi ya pinki na kidumu cha lita 05 kwa ajili ya maji ya kunywa.
- ix. Kwanja 01, jembe 01, brashi 01 kwa ajili ya kusafishia sink la choo na squizer (kikaushio cha maji) 01, sabuni ya unga pakiti 05 kwa ajili ya usafi wa vyoo na bweni kwa wanafunzi wa **PCM.**
- x. Sanduku la chuma au bati.
- xi. Kandambili kwa ajili ya kuogea na sio yeboyebo.
- xii. Sabuni, dawa za meno na mswaki kwa matumizi binafsi.
- xiii. Begi la kubebea daftari.
- xiv. Nguo za kulalia (night dress).
- xv. Kanga pair moja.
- xvi. Tochi au taa ya solar 01 kwa ajili dharura. (tochi za umeme haziruhusiwi).
- xvii. Simple shoes kwa ajili ya mesi.
- xviii. Daftari 12 counter books quire 4, kalamu za bluu au nyeusi box 01.
- xix. Uje na picha (passport size) 02 za wazazi halisi yaani baba na mama au walezi 02 kama huna wazazi pamoja na passport size moja ya mwanafunzi.
- xx. Njoo na faili 02 kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zako.
- xxi. Njoo na kivuli cha cheti cha kuzaliwa pamoja na kivuli cha cheti cha matokeo (reslts slip).
- xxii. Mathematical set, rula ndefu, graph paper za kutosha na calculator aina ya ***CACIO fx 991ms***. (non programmable calculators)
- xxiii. Kila mwanafunzi aje na bima ya afya au shilingi **50,400/=** kwa ajili ya kukata bima ya afya. (**bima ya afya ni lazima**).

*NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA.*

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA  WASICHANA GEITA..

‘***WE ARE LEARNING AND LEADING FOR PROSPERITY’***

……………………………..

MWAMINI G. KAGOMA.

MKUU WA SHULE.

**0759408933/0787708469**

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

**S**heria hizi zinalenga kumpa mwanafunzi **UTII, HESHIMA NA NIDHAMU**, Sheria hizi ni pamoja na:-

1. Mwanfunzi anapaswa kusimama na kusalimia mwalimu, mtu yeyote au kundi la watu wanaomzidi umri popote awaonapo au kukutana nao.
2. Ni marufuku kutumia lugha chafu wakati wowote kwa walimu wao, wao kwa wao na kwa watu wengine.
3. Unatakiwa kuheshimu alama za Taifa, mfano: Bendera ya Taifa,viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
4. Hauruhusiwi kuonekana au kutembelea:-
   i. Vilabu vya pombe.
   ii. Kumbi za starehe.
   iii. Nyumba za kulala wageni (guest houses).
   iv. Nyumba za walimu/watumishi bila ruhusa.
5. Hauruhusiwi kuhalibu mali ya shule.
6. Kuzingatia usafi binafsi na kuhifadhi mazingira ya shule.
7. Hauruhusiwi kupiga kelele ovyo ndani na nje ya madarasa.
8. Unatakiwa kutumia kiingereza daima wakati wote ndani na nje ya darasa.
9. Ni marufuku kabisa kwa mwanafuni:-
   i. kuvuta sigara au kunywa pombe.
   ii. kufuga kucha au kuzipaka rangi.
   iii. kufuga ndevu na nywele ndefu.
   iv. kuvaa mavazi yasiyo ya heshima na kulegeza suruali (kuvaa mtepesho).
   v. kugombana ama kupigana.
   vi. kutoroka darasani wakati wa vipindi au kazini.
   vii. kuiga mitindo ya kihuni, mfano mavazi, kunyoa kipara, n.k.
   viii. kuja na simu au kutumia simu ya mkononi shuleni, ikikamatwa haurudishiwi na utarudishwa nyumbani na utafutwa shule.
   ix. Kuvaa kofia au bangili na mapambo mengine yasiyo ya lazima.
10. Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani na kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote inayotolewa na walimu.
11. Wakati wa kipindi hauruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa.
12. Ni lazima kuvaa sare za shule kila uwapo katika eneo la shule na nje ya shule.

13. Ni lazima kuhudhuria kipindi cha maandalizi ya masomo kwa vipindi vya mchana na usiku (prepo). Mwisho wa maandalizi ya usiku ni 5:00 usiku na unatakiwa uwe umelala na kuzima taa za chumbani ifikapo saa 5:30 usiku.
14. Hauruhusiwi kufungua redio darasani.
15. Ni marufuku kuacha kutandika kitanda chako na kutofanya usafi wa chumba chako.
16. Ni marufuku kupeleka chakula bwenini bila kibali, chakula chote kitaliwa bwaloni/mesini.
17. Ni marufuku kuacha taa zinawaka chumbani wakati wa vipindi darasani.
18. Ni marufuku kujihusisha na vikundi hatarishi vya usalama.
19. Ni marufuku kulala nje ya shule bila ruhusa.
20. Ni marufuku kutoka nje ya shule bila kuomba ruhusa.
21. Unapokuja kuripoti uje na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.
22. Mwenye bima ya afya aje nayo kwa ajili ya matibabu au shilingi **50,400/=** kwa ajili ya kukata bima (**ni lazima kila mwanafunzi awe na bima ya afya**).
23. Hauruhusiwi kuja na suruali (pedal) na nguo zinazofanana na hizo.
24. Ni marufuku kuchelewa kuripoti shuleni baada ya likizo yoyote kumalizika, unapaswa kuripoti shule mara moja baada ya shule kufunguliwa yaani siku ya kufungua shule.

**SHERIA ZA MESINI**.

1. Lazima uwahi wakati wa chakula ili kuepuka kukosa chakula.
2. Usimwage chakula ovyo mezani na sakafuni.
3. Kila mwanafunzi aoshe vyombo vyake vya kulia chakula baada na kabla ya kula.
4. Hauruhusiwi kupiga kelele mesini wakati wa chakula.
5. Baada ya chakula ondoa mabaki yaliyodondoka mezani na chini.
6. Si ruhusa kujipikia.
7. Chakula cha wagonjwa kitashughulikiwa na viongozi wa afya na wale wahusika tu.
8. Ni marufuku kuvaa ndala mesini.
9. Hauruhusiwi kupeleka chakula bwenini.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**NB:- Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi, hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI AU MTOTO WAKO USITUME. NI VYEMA**

**UWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- ✓ **MKUU WA SHULE:- 0759408933.**

**HITIMISHO:-**

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto waendelee na wapate kile wanachokifuata shuleni, yaani elimu. Msisitizo wa bodi ya shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha asilimia 80 au zaidi katika kila somo. Sheria zote hizo zinalenga kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masomo yake.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.


**……………………………..**

**MWAMINI G KAGOMA.**

**MKUU WA SHULE.**

**0759408933/0787708469.**

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.

**M**wanafunzi anatakiwa kujaza nafasi zilizo wazi, aidha anatakiwa kusoma kwa makini maelekezo yaliyoandikwa.

1. Majina matatu ya mwanafunzi:- ..........................................................................................
2. Picha ya mwanafunzi: ..............................................................

| |
|---|
| Picha ya mwanafunzi |

3. Anuani yako kamili: ..........................................................................................................
4. Tarehe ya kuzaliwa .............................. mwezi ............................. mwaka ...........................
5. Mahali ulipozaliwa .............................................................................................................
6. Dini au dhehebu ...................................................................................................................
7. Uraia wako ..........................................................................................................................
8. Jina kamili la mzazi/mlezi wako ...........................................................................................
9. Anuani ya mzazi/mlezi: ........................................................................................................
10. Namba za simu zinazotumika kukupata:-
    i. Baba/mlezi ...................................................................................................................
    ii. Mama .........................................................................................................................
    iii. Ndugu wa karibu ..........................................................................................................
11. Mahali unapoishi kitongoji ............................................., mtaa ............................................ kata ............................................wilaya ................................ mkoa ....................................
12. Jina la balozi wako .............................................................................................................

**AHADI/KIAPO.**

**Mimi** ......................................................................... kwa utashi na akili yangu timamu ninakubali nafasi ya masomo niliyopewa. Nitakuwa tayari kujiendeleza kimasomo, nimesoma na kuzielewa na nitazifuata sheria za shule pamoja na kanuni na taratibu zitakazotolewa. Natambua kuwa nikifukuzwa shule kwa sababu ya kuvunja sheria za shule makusudi nitavunja moyo wa wazazi na wale wote wanaonisaidia, ikiwemo serikali inayonisomesha, hivyo jamii itanidharau kabisa. Naahidi kuwa na utii kwa walimu na wafanya kazi wote waliopo hapa shuleni ili wanipende na kunisaidia zaidi. Sitakuwa tayari kuanzisha, kushuri wala kujihusisha na kushiriki katika vurugu za aina yoyote shuleni, hususani mgomo kwani ni kwenda kinyume na sheria na taratibu za shule. Nitakuwa katika masomo na kazi zote za shule. Nitahudhuria vipindi vyote darasani bila kukosa katika siku zote za masomo na nitaomba ruhusa ninapopata shida.

**MUNGU NISAIDIE.**

| ........................................................... | ............................... | .............................. |
|---|---|---|
| **JINA LA MWANFUNZI** | **SAINI** | **TAREHE** |

## MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI.

Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi.

1. Jina la mzazi/mlezi ..........................................................................................
2. Picha ya mzazi/mlezi .................................................................

| |
|---|
| Picha<br>Ya<br>Mzazi/mlezi |

3. Anwani ya mahali unapoishi ..........................................................................
4. Namba za simu zinazotumika kukupata .....................................................
   i. Baba/mlezi ..............................................................................
   ii. Mama ....................................................................................
   iii. Ndugu wa karibu ......................................................................
5. Mahali unapoishi kitongoji ..............................................., mtaa..............................., kata.........................................., wilaya,............................., mkoa .............................
6. Kazi ya mzazi/mlezi ..........................................................................................
7. Dini au dhehebu ..................................................................................................
8. Uraia ....................................................................................................................
9. Jina la balozi wako ...........................................................................................
10. Ninakubali nafasi aliyopewa mtoto wangu, (jina la mwanafunzi). ............................................................. ...............................................................
11. Nitashirikiana na uongozi wa shule katika suala la kumlea, kumwendeleza na kumtia moyo wa kupenda shule.
12. Nitahakikisha kwamba mtoto wangu anawahi shuleni na pia hachelewi likizoni.
13. Nitafuatilia maendeleo yake kitaaluma kwa karibu zaidi ikiwa ni pamoja na kuonana na walimu wake.
14. Natambua pia kumchelewesha kufika shuleni siku ya kufungua shule kunaweza kusababisha kupoteza nafasi aliyopewa.
15. Nitahakikisha mtoto wangu anahudhuria shuleni kila siku za masomo bila kukosa.
16. Nitahudhuria vikao vya wazazi kwa ajili ya maendeleo ya shule.

**NB: Endapo utahama au kubadili namba za simu tafadhali lete taarifa shuleni ili kubadilisha kumbukumbu zako pia ili kurahisisha mawasiliano.**

**Jina la mzazi/mlezi. ...........................................................................................**

**Saini ya dole gumba ....................................................................**

| |
|---|
| |

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.**

1. Uasherati na ushoga (mahusiano ya jinsi moja).
2. Ubakaji.
3. Wizi.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu makusudi mali ya umma.
7. Kudharau bendera ya taifa.
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha ujauzito.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo, kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kuwa na simu ya mkononi.
14. Utoro wa zaidi ya siku 90 mfululizo bila taarifa.
15. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua au kunywa sumu.
16. Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzake, mwalimu/mlezi na jamii kwa ujumla.
17. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni (guest house).

**SHUGHULI ZA NJE NA DARASANI.**

**U**natakiwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zifuatazo:-

- ✓ Miradi ya shule .
- ✓ Vilabu vya masomo.
- ✓ Utamaduni na michezo.
- ✓ Usafi wa mazingira, madarasani na vyooni.

***KARIBU SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA GEITA.***

‘***WE ARE LEARNING AND LEADING FOR PROSPERITY’***

**...............................**

***MWAMINI G. KAGOMA .***

***MKUU WA SHULE.***

**0759408933/0787708469**

**GOVRENMENT OF TANZANIA.**

**MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To medical officer, ........................................................................................ (name in full).

Please examine the above named student as to his or her physical and mental fitness for a secondary education.

1. Blood count ..............................................................................................................
2. Stool examination ......................................................................................................
3. Urine analysis ...........................................................................................................
4. Venereal disease ........................................................................................................
5. T. B and leprosy test ..................................................................................................
6. Eye sight ...................................................................................................................
7. Hearing .....................................................................................................................
8. Asthma ......................................................................................................................
9. Epilepsy ....................................................................................................................
10. Neuroses ..................................................................................................................
11. Speech .....................................................................................................................
12. Limbs ......................................................................................................................
13. Pregnancy (girls) ......................................................................................................
14. Other serious diseases ..............................................................................................

Remarks and additional information e.g physical defects or impairments, infection, chronic or family disease e.g sickle cell.

..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................

I certify that the above named student is fit/unfit to pursue secondary education.

Signature ............................................................

Designation .........................................................

Station .................................................................

Date and stamp ....................................................